BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 24 Mei, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2025/2026.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

221. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ni ipi nafasi ya wanawake wenye mahitaji maalumu katika suala zima la utekelezaji wa mifumo ya ndani na ya nje ya Haki za Binaadamu.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

116. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ujasiriamali wa kutengeneza vyungu na mikungu si tu kuwa ni sehemu ya ajira lakini pia hulinda milka na silka za Mzanzibari.

Je, Serikali inawaondolea vipi urasimu wa kupata mikopo nafuu wajasiriamali kupitia uwezeshaji na ushirika ili kuweza kujikwamua zaidi na kutimiza malengo yao.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

170. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, ni miradi gani ya kupigiwa mfano ambayo Mhe. Rais inamuweka katika ramani ya kumbukumbu isiyosahaulika, vizazi na vizazi.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

63. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Msimu wa mvua za masika tayari umefika na Wizara yako ina kawaida ya kuwahamasisha wananchi juu ya suala zima la kupanda miti.

(a) Je, Wizara yako inawahakikishia vipi wananchi juu ya kupatikana miche ya miti mbali mbali.

(b) Kuna utaratibu gani wa Wizara yako kutoa miche kwa wananchi mara tu muda wa mvua unapofika.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamatuni na Michezo:**

179. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

(a) Tuna maabara ngapi mpaka hivi sasa za matumizi ya lugha ya Kiswahili.

(b) Kwa kiasi gani maabara hizi zina mchango mkubwa katika makuzi ya lugha ya Kiswahili.

(c) Mchakato wa Sera ya Lugha ya Kiswahili upo vipi kwa sasa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

223. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa mabadiliko ya kimtaala ni safari ya kuandaa kizazi chenye maarifa stadi na umahiri, vipi na kwa mikakati gani Wizara yako itahakikisha kuwa lengo hili linaweza kutimia ipasavyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

230. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia suala la kuanzishwa vyuo vya udereva kwa Unguja na Pemba kwa lengo la kuongeza uelewa kwa wananchi juu ya masuala ya usalama wa barabarani.

(a) Je, mpaka hivi sasa ni vyuo vingapi vya udereva vimeanzishwa kwa upande wa Pemba.

(b) Kwa kuwa kisheria hairuhusiwi kwa mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 kuendesha vyombo vya moto, ni kwa kiasi gani Wizara yako imesimamia suala hili kupitia vyuo hivyo vya udereva.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

295. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Ni lini Wizara yako itaanzisha kozi za Uchumi wa Buluu kama uvuvi, kilimo cha bahari na menejimenti ya uchumi wa buluu ili kuondokana na tatizo la ukosefu wa ujuzi wa matumizi ya rasilimali za Uchumi wa Buluu.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

12. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kuna hoteli katika maeneo mbali mbali hapa Zanzibar zilizojengwa kwa lengo la kuongeza kipato cha wamiliki pamoja na kukuza utalii nchini.

(a) Ni kwa kiasi gani hoteli hizi zinashirikiana na jamii katika maeneo husika ili kuhakikisha maendeleo ya jamii yanapatikana.

(b) Kwa kuwa jamii hizi hutoa maeneo ya vijiji vyao kujengwa hoteli hizo, ni kiwango gani cha mapato hutengwa kwa ajili ya vijiji hivyo.

(c) Ni upi muitikio wa wamiliki wa hoteli hizo juu ya utekelezaji wa dhana ya utalii kwa wote kupitia miradi ya kijamii katika vijiji mbali mbali nchini.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**24 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**WAWAKILISHI, ZANZIBAR**